HALMASHAURI YA WILAYA YA MWANGA
SHULE YA SEKONDARI YA WASICHANA DR. ASHA-ROSE MIGIRO,
S.L.P 259,
MWANGA.

Blog: www.migirosec.blogspot.com
Email:dr.asharosemigirosec@yahoo.com
Mobile +255 768 378 604

Kumb. Na.DR.ARM/GSS/KS/KI/2019/VOL I/2/12 **01/12/2020**

Jina la Mwanafunzi .....
S.L.P.....
Namba ya simu ya Mzazi/Mlezi.....

YAH: MAAGIZO YA KUJIUNGA NA SHULE YA SEKONDARI YA WASICHANA DR.ASHA-ROSE MIGIRO, MWAKA -2021.

1.0 UTANGULIZI.
Kwa niaba ya Bodi ya shule ninayo furaha kukuarifu kuwa umechaguliwa kujiunga na kidato cha kwanza katika shule hii mwaka 2021.
Shule ya sekondari ya wasichana Dr.Asha-Rose Migiro ipo umbali wa km 4 kutoka makao makuu ya Halmashauri ya Wilaya.

Usafiri wa taksi unapatikana katika kituo cha mabasi cha Mwanga.

Muhula wa kuanza masomo unaanza tarehe **11/01/2021** unatakiwa kuripoti shuleni tarehe **11/01/2021.**

2.0 MAMBO MUHIMU YA KUZINGATIA
2.I SARE YA SHULE.
Mzazi/Mlezi unapaswa kumpatia mwanao sare ya shule kama maelekezo yanavyoonyesha hapo chini:-

i) Mashati mawili meupe, mikono mifupi,
ii) Sketi mbili za rangi ya **ugoro(dark brown)** ndefu chini ya goti yenye **marinda 10** ya kawaida. Kitambaa kizito**, sampuli ya kitambaa imeambatanishwa**
iii) Tai moja ya rangi ya **ugoro na mistari meupe, Sampuli inapatikana shule**
iv) Viatu vya **ngozi vyeusi vya kufunga kamba** vyenye kisigino kifupi.
v) Soksi nyeupe ndefu pea mbili.
vi) Sweta la rangi ya **ugoro (dark brown) sampuli inapatikana shule**

2.2 SARE YA HOSTEL
Mzazi/Mlezi unapaswa kumpatia mwanao sare ya hosteli na vifaa vya malazi kama maelekezo yanavyoonyesha hapo chini:

(i) Gauni mbili ndefu mshono wa solo pana yenye shingo duara na isiyo na mikanda kiunoni, **sampuli ya kitambaa imeambatanishwa**
(ii) Shuka mbili (shuka moja ya rangi ya pinki,na nyingine ya rangi ya blue bahari)
(iii) Blanketi moja aina ya velvet
(iv) Tracksuit ya rangi ya bue bahari.
(v) Tishirt moja nyeusi.
(vi) Neti ya pande nne (square) kwa ajili kujikinga na mbu

Mzazi/Mlezi tafadhali zingatia aina ya sare iliyoainishwa hapo juu. Mwanafunzi atakayeripoti na sare tofauti na zilizoainishwa atalazimika kushona sare zingine. Sare zote na vifaa vyingine vitakaguliwa siku ya kuripoti shule, kwa hiyo Mwanafunzi avae sare kamili ya shule kuanzia siku ya kuripoti shule.

2.3. VIFAA KWA AJILI YA TAALUMA

i) Daftari kubwa zisizopungua 10, Kalamu ya wino (blue/black pen) Penseli na Rula

ii) Mkebe wa vifaa vya Hisabati (Mathematical set)

2.4. VIFAA VINGINE (Mahitaji ya kibinadamu)

Mzazi/Mlezi unapaswa kumpatia mwanao vifaa vilivyoainishwa hapo chini kwa ajili ya matumizi yake akiwa hostel.

(i) Kanda mbili pea moja
Vitenge vipande viwili

(ii) Mswaki na dawa ya meno

(iii) Mafuta ya kujipaka aina ya Vaseline Petrolium Jelly

(iv) Sabuni za kuogea zinazoshauriwa ni medicated soap ambazo hazing'arishi wala kuchubua ngozi. Aidha sabuni za kufulia ni sabuni za mche na sabuni za unga.

(v) Shuka mbili za kulalia moja ikiwa nyeupe isiyo na maua

(vi) Kufuli la kufungia kabati lake

(vii) Ndoo ndogo kwa ajili ya matumizi yake binafsi.

Sanduku za bati /chuma hazitakiwi shule,mwanafunzi aje na sanduku dogo lisilo la chuma.
Sampuli inapatikana shule

2.5 VIFAA KWA AJILI YA UTUNZAJI WA MAZINGIRA.

i) Ndoo ndogo moja .

ii) Ufagio moja aina ya Ukindu

2.6. VIFAA VYA CHAKULA

Sahani moja na kijiko.

MICHANGO YA HOSTEL

NA	MICHANGO	MUHULA WA I	MUHULA WA II	JUMLA KWA MWAKA
1	Chakula	163,000/=	163,000/=	326,000/=
2	Taaluma	15,000/=	-	15,000/=
3	Posho watumishi wasio walimu	13,000/=	12,825	25,825/=
4	Matibabu	5,000/=	5,000/=	10,000/=
5	Maji	2,500/=	2,500/=	5,000/=
6	Umeme	6,000/=	6,000/=	12,000/=
7	Uendeshaji Gari	7,000/=	6,500/=	13,500/=
8	Ujenzi wa Bweni	50,000/=	50,000/=	100,000/=
9	Ukarabati wa miundombinu	10,000/=	10,000/=	20,000/=
10	Utunzaji wa Mazingira	1000/=	-	1,000/=
	JUMLA	**272,500/=**	**255,825/=**	**528,325/=**

Malipo yafanyike kupitia Akaunti ya shule Namba 40201200057 NMB,
Mzazi/Mlezi alete Pay in Slip Mwanafunzi anapo ripoti shule.

SHERIA NA KANUNI MUHIMU ZA SHULE.

Shule inaendeshwa kwa mujibu wa Sheria ya Elimu Na 25 ya Mwala 1978 na kama ilivyorekebishwa kwa sheri Na 10 ya Mwaka 1995. Aidha inazingatia miongozo yote inayotolewa na Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi, yenye dhamana ya Elimu nchini na ofisi ya Waziri Rais TAMISEMI yenye jukumu la Usimamizi na Uendeshaji wa Elimu. Unatakiwa kuzingatia mambo ya msingi yafuatayo ambayo yatafafanuliwa kwa maandishi na utapewa nakala yake baada ya kuripoti shuleni .

a) Heshima kwa Viongozi, Wazazi, Wafanyakazi wote ,Wanafunzi wengine na jamii kwa ujumla ni jambo la lazima
b) Mahudhurio mazuri katika kila shughuli ndani na nje ya shule kulingana na ratiba ya shule ni lazima
c) Kushiriki kwa makini kufanya maandalio ya jioni (preparation)
d) Kuwahi katika kila shughuli za shule na nyingine utakazopewa.
e) Kufahamu mipaka ya shule na kuzingatia kikamilifu maelekezo juu ya kuwepo ndani na nje ya mipaka hiyo wakati wote wa uanafunzi wako katika shule hii
f) Kutunza usafi wa mwili, mavazi na mazingira ya shule
g) Kuvaa sare ya shule wakati wote unapotakiwa
h) Kuzingatia ratiba ya shule wakati wote
i) Kutunza mali za umma

MAKOSA YAFUATAYO YANAWEZA KUSABABISHA KUFUKUZWA AU KUSIMAMISHWA SHULE.

a) Wizi
b) Uasherati na ushoga
c) Ubakaji
d) Ulevi na matumizi ya madawa ya kulevya kama vile uvutaji wa Bangi, Cocaine,Mirungi ,Kubeli na kadhalika.
e) Kupigana na kupiga
f) Kuharibu kwa makusudi mali ya umma
g) Kudharau Bendera ya Taifa
h) Kuwa mjamzito/kupata mimba
i) Kuoa au kuolewa
j) Kutoa mimba
k) Kugoma, kuchochea na kuongoza au kushiriki kuvuruga amani na usalama wa shule au watu
l) Kukataa adhabu kwa makusudi
m) Kuwa na simu ya mkononi au simcard

"KARIBU SANA KATIKA SHULE YAKO"

Flaviana S Sumawe
Mkuu wa Shule

Headmistress
Dr-Asha-Rose Migiro Gss
P.O.Box 259-Mwanga